TANGAZO LA SERIKALI NA. 748 la tarehe 23/8/2024

SHERIA ZA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA MAZAO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA, 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauiri" maana yake ni Halmashauiri ya Wilaya ya Muheza.

"mazao" maana yake ni mavuno ya shambani au maliasili au mazao ya baharini yanayozalishwa au yanayoingizwa kwenye soko au ndani ya eneo la mamlaka ya Halmashauri.

"mazao ya chakula" maana yake ni mazao yote ya chakula ambayo yatatumika kwa madhumuni ambayo si ya kibiashara;

"mazao ya biashara" ni mazao yote ambayo hata kama ni ya chakula lakini yatatumika kwa wakati husika kwa madhumuni ya biashara;

"mfanyabiashara" -
(a) ni mtu yeyote anayeuza bidhaa sokoni au gulioni kwa jumla au rejareja;
(b) linapotumika kuhusiana na mkulima maana yake ni mkulima yeyote ambaye anajihusisha na shughuli ya kuuza mazao kama atakavyoyatoa shambani kuyapeleka sokoni;
(c) linapotumika kuhusiana mnunuzi ina maana ya mtu yeyote anayejihusisha na shughuli ya kuuza mazao kama atakavyoyanunua kutoka kwa mkulima au mtu yeyote kutoka katika eneo la Halmashauri;
(d) linapotumika kuhusiana na mmiliki wa mashamba makubwa ina maana ya mmiliki huyo kutumia mazao hayo kama malighafi katika kiwanda cha mmiliki husika kwa kiwango kilekile alichovuna katika shamba husika;
(e) linapotumika kuhusiana na Taasisi ya Umma au Serikali au ya Mtu binafsi au Kampuni ina maana ya Taasisi au Kampuni hiyo inayojihusisha na kilimo cha mazao hayo;

"mkulima" maana yake ni mtu yeyote ambaye anajishughulisha na shughuli za kilimo katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri;

"Mwenyekiti"-
(a) linapotumika kuhusiana na Halmashauri ya Wilaya maana yake ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya;
(b) linapotumika kuhusiana na Kijiji, maana yake ni Mwenyekiti wa Kijiji;
(c) linapotumika kuhusiana na Kitongoji, maana yake ni Mwenyekiti wa kitongoji;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnunuzi" maana yake ni mtu yeyote anayenunua mazao na tafsiri hii itajumuisha mkulima anayefanya biashara ya mazao kutoka shambani kupeleka sokoni;

"ushuru" maana yake ni ushuru wa mazao utakaotozwa na

Halmashauri baada au kabla ya kupata huduma.

Utozaji wa ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ushuru wa mazao kwa kiwango cha asilimia tatu ya bei ya kununulia mazao utakaolipwa na mnunuzi wa mazao kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) na kwa madhumuni ya ukusanyaji wa ushuru kutoka kwa Shirika, Kampuni, Taasisi za Serikali au Taasisi binafsi ambazo zinamiliki mashamba makubwa, Halmashauri itatoza ushuru huo kwa kiwango cha asilimia tatu kwa bei ya kununulia mazao hayo, na kwa utaratibu wa malipo kama utakavyopangwa na Bodi inayosimamia mazao husika kiasi ambacho kitatozwa kutoka kwa Kampuni.

(3) Kwa madhumuni ya kurahisisha ukusanyaji wa ushuru, mara baada ya mlipa ushuru kuchukua mazao yake atalazimika kuchukua hati ya kusafirisha mazao kutoka Halmashauri inayothibitisha kiasi cha mazao anachosafirisha ukilinganisha na kile alicholipia ushuru.

(4) Bila kuathiri kanuni ndogo za (1), (2) na (3), ushuru wowote utakaotozwa utatozwa kwa kuzingatia uzito na si ujazo wa gunia.

Uteuzi wa Wakala

5.-(1) Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kuteua Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu-

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri;

(c) kuwasilisha makusanyo yote anayowajibika kukusanya kwa kuzingatia mkataba alioingia na Halmashauri;

(d) kutoa taarifa kwa Halmashauri kuhusiana na mtu yeyote ambaye kwa makusudi amekataa au

ameshindwa kulipa ushuru husika;

(e) kuwasilisha Halmashauri orodha ya wanunuzi wote aliowakusanya ushuru katika eneo aliloteuliwa kukusanyia ushuru huo

(3) Mkusanya ushuru atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii endapo:

(a) atashindwa bila sababu ya msingi kuwasilisha kiwango cha fedha alichokusanya kutoka kwa wanunuzi wa mazao;

(b) atakuwa anafahamu kiwango kinachostahili kutozwa kutoka kwa mnunuzi na kwa makusudi akakusanya zaidi ya kiwango husika;

(c) kwa makusudi akiwasilisha kiwango cha mawasilisho pungufu ukilinganisha na stakabadhi za malipo na orodha ya wanunuzi aliowaorodhesha; na

(d) kwa makusudi akishindwa kutekeleza lolote analowajibika kulitekeleza kitendo ambacho kitaathiri mapato hayo.

Ushuru wa mazao ya misitu

6.-(1) Halmashauri itatoza ushuru wa mazao ya misitu kutoka kwa mnunuzi wa mazao ya misitu kwa kiwango cha asilimia tatu ya bei ya kununulia au ya kuuzia mazao hayo.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), mazao ya misitu yatajumuisha mazao ya misitu timbao na mazao ya misitu ambayo si timbao kama inavyoonekana katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(3) Kwa madhumuni ya urahisi wa ukusanyaji wa ushuru wa mazao ya misitu inayomilikiwa na Taasisi ya Umma, Mtu binafsi au Kijiji, muuzaji huyo atawajibika kutoa ushirikiano kwa Halmashauri ili isipoteze ushuru unaopaswa kulipwa na mnunuzi husika;

(4) Halmashuri inaweza kumteua kwa maandishi Mtu yeyote katika Taasisi inayohusika na uuzaji wa mazao ya misitu kukusanya ushuru wa mazao ya misitu kwa niaba ya Halmashauri na kuwasilisha kiasi kilichokusanywa kwa Halmashuri.

(5) Taasisi inayomiliki mazao ya misitu itakuwa na wajibu wa kutoa taarifa kwa wanunuzi kuwa wanawajibika chini ya Sheria Ndogo hii kulipa ushuru wa

mazao ya misitu kwa Halmashauri au kutoa taarifa kwa Halmashauri kuwa Taasisi husika inatarajia kuuza mazao ya misitu au kuainisha pamoja na bei watakayomtoza mnunuzi wa mazao ya misitu gharama ya ushuru ambao mnunuzi anawajibika kuwasilisha Halmashauri na kuwasilisha kiasi cha ushuru unaotakiwa kwa Halmashauri.

Wajibu wa kutumia vipimo sahihi

7.-(1) Kila mfanyabiashara, mkulima au mtu yeyote atakayehusika na biashara ya mazao au ubebaji wa mazao atakuwa na wajibu wa kutumia vipimo sahihi katika ubebaji wa mazao hayo.

Sura ya 340

(2) Kila mfanyabiashara, mkulima au mtu yeyote atakayefungasha mazao anawajibika kufungasha mazao kwa kuzingatia Sheria ya Vipimo na kanuni za ufungishaji wa Bidhaa.

Eneo la kuuza na kununulia mazao

8.-(1) Pale ambapo itatokea umuhimu wa kuuza mazao tofauti na shambani, mazao yote yatauzwa katika maeneo ambayo Halmashauri itaelekeza.

(2) Ni marufuku kwa mfanyabiashara, mkulima, au mtu yeyote:

(a) kuuza mazao ambayo hayajakomaa, kupepea mazao au kuyachemsha kwa lengo ya kuyakomaza au kufanya jambo lolote ambalo litaathiri ubora wa mazao hayo; au

(b) kuuza mazao katika eneo ambalo halijaelekezwa na Halmashauri.

(3) Halmashauri itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa katika maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya kuuza na kununua mazao ya kilimo kunakuwepo na mzani utakaotumika uliohakikiwa na wakala wa vipimo.

Adhabu kwa utoroshaji mazao

9.-(1) Halmashauri itamtoza ushuru mnunuzi wa mazao endapo mazao yaliyonunuliwa yatakamatwa kuwa hayajalipiwa ushuru na ikithibitika mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru anaodaiwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), endapo mnunuzi atashindwa kulipia ushuru anaodaiwa, mazao yake yatakamatwa na kuhifadhiwa kwa masaa kumi na mbili na baada ya muda huo kupita bila ya

mnunuzi kuyakomboa mazao hayo yatauzwa kwa mnada au kugawiwa kwa taasisi za Serikali baada ya kupata kibali cha Mahakama.

(3) Fedha zitakazopatikana baada ya mauzo ya mazao yaliyokamatwa na kunadiwa chini ya kanuni ndogo ya (2), Halmashauri itachukua ushuru wake, gharama za utunzaji wa mazao kwa wakati wote mazao yalipokuwa chini ya uangalizi wa Halmashauri pamoja na gharama za mnada na kiasi kitaka chobaki atarudishiwa mnunuzi.

Mazao kupoteza thamani

10. Endapo mazao yaliyokamatwa chini ya kanuni ya (9) yatapoteza thamani, Halmashauri haitahusika na upotevu wa thamani kwa mazao yaliyokuwa chini ya uangalizi wake.

wajibu wa kutoa taarifa

11.-(1) Mtu yeyote ambaye anawajibika kutoa taarifa kuhusiana na malipo ya ushuru anawajibika kutoa taarifa hizo kama alivyotarajiwa kwa Halmashauri, Kijiji, mkusanya ushuru, Wakala au Kamati ya ukasimiaji ushuru iliyoundwa chini ya Sheria kwa madhumuni ya kukasimia kiwango cha ushuru au ukusanyaji ushuru.

(2) Kwa madhumuni ya kupata taarifa chini ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri, Kijiji, mkusanya ushuru, Wakala au Kamati ya ukasimiaji ushuru kwa kadiri itakavyokuwa anayehusika na utoaji wa wito huo, inaweza kumuita mtu yeyote kufika mbele yake katika muda na mahali ambapo pametajwa katika barua ya wito.

Kukusanya ushuru bila ruhusa

12. Mtu yeyote ambaye:
(a) hajaruhusiwa na Halmashauri au Kijiji kwa maandishi kukusanya ushuru unaokusanywa chini ya Sheria Ndogo hii;na
(b) amekusanya au amejaribu kukusanya ushuru kwa kiwango ambacho hakijatajwa chini ya Sheria Ndogo hii,

anatenda kosa chini ya Ndogo hii.

Makosa kwa kukataa kutoa taarifa

13.-(1) Mtu yeyote ambaye atatakiwa kutoa taarifa chini ya Sheria Ndogo hii:
(a) kwa makusudi akatoa taarifa ya uongo au amejaribu kutoa taarifa ya uongo kwa

Halmashauri, Kijiji, Wakala, mlipa ushuru au Kamati ya ukasimiaji ushuru, juu ya suala lolote linalohusiana na ukusanyaji ushuru; au
(b) amedharau, amekataa au bila ya sababu za msingi ameshindwa kutoa taarifa zinazotakiwa,

atakuwa anatenda kosa.

(2) Mtu yeyote ambaye ametakiwa kufika mbele ya Halmashauri, Kijiji, mkusanya ushuru, Wakala au Kamati ya ukasimiaji ushuru na hajafanya hivyo, anatenda kosa.

Halmashauri kuchukua hatua za kisheria

14. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kufungua shauri la jinai kuhusiana na malipo ya ushuru au adhabu kwenye Mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza shauri hilo, endapo kufanya hivyo hakutaathiri haki ya mtu yeyote au Mamlaka nyingine ya kufungua shauri la jinai chini ya Sheria Ndogo hii.

Makosa

15. Mtu yeyote ikiwa ni mnunuzi, muuzaji, wakala au mkusanya ushuru anatenda kosa endapo:

(a) atashindwa, atadharau, au atakaidi kulipa ushuru chini ya Sheria Ndogo hii;
(b) atashindwa, atadharau, au atakaidi kuwasilisha ushuru aliokusanya kwa Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii;
(c) atakusanya ushuru bila kuwa na kibali cha kukusanya ushuru;
(d) atashindwa, atadharau au atakaidi kuwasilisha taarifa au atatoa taarifa za uongo ambazo zinahitajika kuthibitisha makusanyo ya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(e) atamshawishi mtu yeyote asilipe ushuru au kumzuia mkusakusanya ushuru kufanya kazi yake;
(f) atashindwa kuhifadhi kumbukumbu ikiwa ni pamoja na rejesta ya mazao na mahesabu yanayohitajika chini ya Sheria Ndogo hii; au
(g) atadanganya, kuhusiana na kitendo chake hicho ataikosesha Halmashauri mapato kama ilivyokusudiwa.

Adhabu

16. Mtu atakayekwenda kinyume na masharti katika Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa faini ya kiasi kisichopungua Shilingi laki mbili na kisichozidi Shilingi Milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufifilisha kosa

17. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha Shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS. Na. 299 la 2008

18. Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ya Mwaka 2010 inafutwa.

---

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

SEHEMU YA I:

USHURU WA MAZAO YA CHAKULA NA BIASHARA

| NAMBA | AINA YA MAZAO | MAELEZO | KIASI CHA USHURU USHURU (SHILINGI) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mazao ya chakula | Mazao yanayotumika kwa chakula na matunda tu | 3% ya bei ya kununulia mazao shambani |
| 2. | Mazao ya biashara | Mazao yanayotumika kwa biashara (karafuu, pilipili manga, mdalasini, chai, kokoa, korosho, na yanayohusiana) | 3% ya bei ya kununulia mazao shambani |

SEHEMU YA II:
Ushuru wa Mazao ya Misitu Timbao

| NAMBA | ZAO | AINA YA ZAO | USHURU |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mbao, magogo, mkaa, kuni, fito, nguzo | Zao la msitu timbao Mrahaba wa mapato ya maduhuli ya mazao ya misitu ya asili [leseni/mauzo] | 3% ya bei ya kununulia |

SEHEMU III:
USHURU WA MAZAO YA MISITU ISIYO MBAO

| NAMBA | ZAO | AINA YA ZAO | KIASI CHA USHURU (SHILINGI) |
|---|---|---|---|
| 1. | Uyoga, asali, nta, utomvu, mbenu, ukindu, kamba, madawa ya mitishamba, masambu | Zao la msitu isiyo timbao | 5% ya bei ya kununulia |

SEHEMU IV:

Ushuru wa Shughuli za Uvuvi

| NAMBA | ZAO | KIASI CHA USHURU (SHILINGI) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa samaki mnadani | 5% ya bei ya kununua samaki mnadani |
| 2. | Leseni ya uvuvi | Kulingana na viwango vilivyotolewa na Serikali Kuu |
| 3. | Leseni ya usajili wa vyombo vya kuvulia samaki | Kulingana na viwango vilivyotolewa na Serikali Kuu |

---

JEDWALI LA PILI

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 17)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFILILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. Mwaka ……… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina……………………….……………………….. Saini…………………………

MBELE YANGU:
Jina: …………………………………..……………………
Saini………………………..………………………..………
Wadhifa: …………………………………………………………
Tarehe……………………………………………………….…

Lakari ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 29 mwezi 07 Mwaka 2022 na lakari hiyo ilibandikwa mbele ya;-

DR JUMAA MOHAMED MHINA,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya Muheza*

ERASTO JEROME MHINA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya Muheza*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*